**UFAHAMU WA KUSOMA**

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu swali la 1 hadi la 4.**

Hapo zamani, wanyama kuishi pamoja halikuwa tukio la ajabu. Walilima, wakavuna na kulea watoto wao pamoja vilevile walikula pamoja walichovuna. Walialikana katika shughuli zote za kifamilia. Wachoyo kama vile Fisi walibadili hulka zao na kuanza kuwahusisha wenzao katika sherehe na shughuli zote za kifamilia.

Siku moja, bintiye Fisi alifuzu katika taaluma ya upishi. Familia ya Fisi ilimwandalia binti yao karamu ya kumtuza na kumpongeza kwa ufanisi huo wa ajabu. Wanyama wote walialikwa, walijawa na bashasha kwa mwaliko waliopata. Miongoni mwa waliofurahia zaidi alikuwa Sungura.

Siku ya siku ilipofika, kila mmoja alishika njia kuelekea kwa Fisi. Sungura ndiye aliyekuwa wa kwanza kuwasili akifuatwa na Mbweha aliyevalia koti nyeusi, shati jeupe na tai yenye milia mieupe na mieusi. Kichwani, chepeo nyekundu ilifunika kichwa chake sawasawa.

Fisi aliwakaribisha kwa shangwe na nderemo kutokana na tajriba ya bintiye katika mapishi, wageni waliandaliwa vyakula vya kurambisha vidole. Baada ya maakuli, kipindi cha kutoa zawadi kilifuatia. Wapo waliompa viungo vya mapishi na vifaa vya kupikia. Kuna waliomzawadi ovaroli, visu na uma za kulia.

Hatimaye, Mbweha alisimama na kutoa shukrani. Ghafla bin vuu Ngiri alijitokeza. Alikuwa akitabasamu huku amebeba sufuria kubwa. Wanyama waliangalia kwa mshangao mkubwa. Sungura alivunjika mbavu kwa kicheko.

1. Andika methali moja inayoafiki maelezo ya aya ya kwanza?

   ______________________________________________________________________

2. Kiini cha sherehe iliyoandaliwa kilikuwa nini?

   ______________________________________________________________________

3. Hadithi hii imeonyesha kwamba wageni waliandaliwa chakula kitamu. Andika mfano mmoja kutoka kwenye kifungu kuthibitisha kauli hii.

   ______________________________________________________________________

   ______________________________________________________________________

4. Je, unadhani ni nani aliyepika chakula kilichoandaliwa wageni?

   ______________________________________________________________________

   ______________________________________________________________________

**UFAHAMU WA KUSOMA**

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu swali la 5 hadi la 8.**

Manufaa ya miti ni mengi sana hasa kwa wanadamu na wanyama. La kutia moyo ni kuwa mwanadamu anayefaidika kutokana na miti ndiye huyu huyu anayekata miti ovyo ovyo kwa ajili ya ubinafsi wake.

Kutokana na miti, sisi hupata vyakula kama vile matunda, mboga, nafaka na hata mizizi kama vile karoti na mihogo. Pia, kuna miti inayotupatia dawa. Maarufu ni mwarubaini ambayo inasemekana kutibu magonjwa arubaini. Basi ni kwa nini tusihifadhi miti ndipo tuangamize maradhi?

Miti pia husababisha harufu nzuri kwenye mazingira. Manukato kutoka kwa miti kama vile mwaridi, mkilua, muasumini na mlangilangi hunukia vizuri mno. Isitoshe miti pia hutupa vivuli na kutupatia mbao ambazo tunatumia kwa manufaa ya ujenzi.



Miti ni makazi ya wanyama. Wanapoishi pale hula chakula kitokanacho na miti. Wako wale wanaoishi mitini na wale wanaojificha vichakani kama vile chui, nyoka na nyani. Ndege na wadudu pia ni mojawapo ya wanaofaidika na miti.

Unapokata miti basi jua kwamba unajinyima haki na kutendea viumbe wengine dhuluma kuu. Tugutukeni na tuache kujichimbia kaburi litakalomeza sisi pamoja na vizazi vyetu.

5. Taja viumbe wanaofaidika kutokana na miti.
   ______________________________________________________________________
   ______________________________________________________________________
6. Kulingana na kifungu ni lipi si faida ya miti?
   A. Hutupa chakula.
   B. Husababisha mafuriko.
   C. Makao ya wanyama, ndege na wadudu.
   D. Asili ya dawa.
7. Kifungu kinasema, "Basi ni kwa nini tusihifadhi miti ndipo tuangamize maradhi?" Mwandishi ana wito gani?
   ______________________________________________________________________
   ______________________________________________________________________
8. Kisawe cha neno manukato ni ______________________________.

**UFUPISHO**

**Soma kifungu hiki kisha ujibu maswali 9 hadi 12.**

Mazingira ni jumla ya maliasili yanayomzunguka mtu, mito, miti, wanyama na majumba ni sehemu muhimu ya mazingira. Uhifadhi wa mazingira ni jambo muhimu mno kwani huu ndio mujibu wa binadamu tangu enzi za Adamu. La ajabu ni kuwa, watu tunaoishi karne hii ya ishirini na moja tumepuuzilia mbali jukumu letu.

Tumegeuka chachandu kujikaanga kwa mafuta yetu wenyewe. Uchafuzi umepita mipaka. Mito, misitu na maziwa hajasazwa kuchafuliwa. Mazingira sasa yanachukiza mno.

Kama hayapendezi! Wapo waja wanaodai kuwa wao hawategemei mazingira kuishi. Hizi ni ndoto za alinacha. Dhana hizi ni potovu na hazina mashiko yeyote. Kumbuka mwenzangu kikulacho ki nguoni mwako na tusipojihadhari tutaangamia kutokana na mazingira machafu. Magonjwa yatokanayo na mazingira machafu yameongezeka.

Magonjwa haya yanatisha mno. Suluhu li wapi? Mkononi mwetu. Tusikubali kuangamia kwa sababu ya utepetevu wa uhifadhi wa mazingira yetu. Sheria zifaazo zinafaa kutungwa ili ziwe silaha dhidi ya uharibifu huu. Watakaovunja sheria watiwe mbaroni, wafikishwe mahakamani na kufunguliwa mashtaka. Hili litakuwa funzo tosha kwa wengine wenye tabia hii chafuzi.

9. Andika habari kuu inayojitokeza katika aya ya kwanza kwa sentensi moja.
______________________________________________
______________________________________________
______________________________________________



10. Fupisha aya ya pili kwa maneno yasiyozidi saba.
______________________________________________
______________________________________________

11. Andika ujumbe wa kifungu kizima kwa sentensi moja.
______________________________________________
______________________________________________

12. Andika kichwa kinachofaa kwa kifungu hiki.
______________________________________________
______________________________________________

**SARUFI**

**Soma kifungu kifuatacho. Kina nafasi 13 hadi 17. Umepewa majibu manne. Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya yale uliyopewa.**

Maliasili **13** yana manufaa **14** kwelikweli. Baadhi ya maliasili ni kama vile **15** wanyamapori, bahari, misitu na **16**. Tutunze maliasili vyema. Wanaoharibu maliasili wanapaswa **17** ili liwe funzo kwa wengine walio na mawazo ya kuyaharibu.

13. A. injini
    B. inchini
    C. nchi
    D. nchini
14. A. makubwa
    B. kubwa
    C. nyingi
    D. wengi
15. A. ;
    B. .
    C. :
    D. !
16. A. ingineyo
    B. mengineyo

C. mengineo
D. nyingineyo

17. A. kutiwa makali
B. kutiwa adhabu
C. kutiwa adabu
D. athabu

**Kuanzia swali la 18 hadi la 27, jibu swali kulingana na maagizo.**

18. Mwakio walimwamkua Talia, "Sabalkheri rafiki yangu?"

Unafikiri walikutana wakati gani?

______________________________________________________________



19. Ni nini ukubwa wa sentensi ifuatayo:

Mtoto yule anasoma kitabu cha hadithi.

______________________________________________________________

20. Tunga sentensi ukitumia maneno yafuatayo ili kuyatofautisha thumni / madhumuni.

______________________________________________________________

__________________________________________________________

21. Je, nomino za majina ya vitu visivyoweza kuonekana au kushikika kwa mikono huitwaje?

______________________________________________________________

__________________________________________________________

22. Jaza nafasi iliyoachwa kwa kinyume cha neno lililopigiwa mstari.

Mwenda na omo marejeo ni **ngamani**.

______________________________________________________________

23. Kamilisha sentensi kwa kugeuza kitenzi kilicho kwenye mabano kiwe katika kauli ya kutendwa:

Mkate uli_______________ vyema na kiwanda cha kutengeneza mikate (oka)

24. Chagua nomino iliyo katika kundi tofauti kutoka kwenye kadi hii.

[Mchanga, Sukari, Mafuta, Mimea]

_____________________________________________

25.Andika sentensi hii katika hali ya masharti - ki-.

Kamaliza angeingia darasani mapema angeandika insha

______________________________________________________________________

26.Sentensi:

"Kipchoge ni duma katika riadha" imetumia mbinu gani ya lugha?



______________________________________________________________________

27.Kamilisha methali:

Kofi hazilii ______________________________

**FASIHI**

28.**Soma wimbo ufuatao kisha ujibu maswali:**

Cha kutumaini sina
Ila damu yake Bwana
Sina wema wa kutosha
Dhambi zangu kuziosha
Kwake Yesu nasimama
Ndiye mwamba ni salama
Ndiye mwamba ni salama
Njia yangu iwe ndefu
Yeye hunipa wokovu
Mawimbi yakinipiga
Nguvu zake ndizo nanga
Damu yake na sadaka
Nategemea daima
Yote chini yakiisha
Mwokozi atanitosha
Nikiitwa hukumuni
Rohoni nina amani
Nikivikwa haki yake
Sina hofu mbele zake

a) Wimbo huu ni wa aina gani?

______________________________________________________________________

b) Eleza sifa tatu za wimbo wa aina hii zinazojitokeza

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

c) Tambua mazingira mawili ambapo nyimbo za aina hii huimbwa

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________



d) Tambua mafunzo kuhusu Yesu

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

e) Taja mhusika mmoja katika wimbo

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

**DONDOO**

29.Soma kifungu hiki kisha ujibu maswali:

Kifo cha mama kiliniumiza sana kwa siku nyingi zilizofuata. Nilikuwa kama mgomba wenye mkungu wa ndizi uliokosa nguzo ya kuuhimili. Nilikesha siku nyingi nikimwaza mama yangu. Pia, nilimwaza baba japo kidogo. Licha na yeye kuwa nduli, nilitamani japo siku moja nikutane naye ana kwa ana. Damu ni nzito kuliko maji ati. Nililaani bahati yangu mbaya duniani. Niliona kuwa kwa namna fulani maisha yalinionea. Nilipoona vijana wenzangu pale Gera, nilitamani ningalikuwa wao. Walikuwa wakicheza na kufurahia maisha. Nilitamani maisha yao. Nilijiuliza kwa nini nilizaliwa nchini Doneka. Mbona sikuzaliwa nchini Tereka, Gandua, Yenka au Azania ambako amani ilikuwa imedumu? Kifo cha mama yangu kiliumiza sana. Sikuwa na matumaini yoyote ya maisha bora. Hata hivyo, kitabu changu Mshale wa Matumaini, kilibaki kuwa liwazo kwangu. Nilikisoma kila wakati.

a) Andika mandhari inayojitokeza

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

b) Eleza sifa tatu za mwandishi

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

c) Fafanua mafunzo matatu

d) Eleza mbinu tatu za lugha



**INSHA**

**Andikia rafiki yako barua ukimwalika kusherehekea siku yako ya kuzaliwa. (Alama 20)**

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

**Learner's sign: ____________________________.**

**Guardian's sign: ___________________________.**

**Date completed: ___________________________.**



MAJIBU

UFAHAMU WA KUSOMA

*1.*

Methali: Kidole kimoja hakivunji chawa.

*2.*

Sherehe iliandaliwa ili kumpongeza binti ya Fisi kwa kufuzu katika taaluma ya upishi.

*3.*

Mfano:
"Wageni waliandaliwa vyakula vya kurambisha vidole."

*4.*

Aliyepika chakula ni binti ya Fisi kwa sababu alikuwa amefuzu katika taaluma ya upishi.

UFAHAMU WA KUSOMA WA PILI

*5.*

Viumbe wanaofaidika kutokana na miti ni:

- Wanadamu
- Wanyama
- Ndege
- Wadudu

*6.*

Jibu: B. Husababisha mafuriko.

*7.*

Mwandishi anatoa wito wa kuhifadhi miti ili kuzuia magonjwa na kulinda mazingira.

*8.*

Kisawe cha neno *manukato* ni marashi au harufu nzuri.

UFUPISHO

*9.*

Habari kuu ya aya ya kwanza ni kwamba uhifadhi wa mazingira ni muhimu sana kwa maisha ya binadamu.

*10.*

Aya ya pili kwa maneno yasiyozidi saba:
Uchafuzi wa mazingira umeenea sana.

*11.*

Ujumbe wa kifungu kizima:
Wanadamu wanapaswa kuhifadhi mazingira ili kuepuka madhara na magonjwa.



*12.*

Kichwa kinachofaa:
Uhifadhi wa Mazingira

SARUFI

*13.*

Jibu: D. nchini

*14.*

Jibu: A. makubwa

*15.*

Jibu: C. :

*16.*

Jibu: B. mengineyo

*17.*

Jibu: B. kutiwa adhabu

MATUMIZI YA LUGHA

*18.*

Walikutana wakati wa asubuhi.

*19.*

Ukubwa wa sentensi:
Ni sentensi kamili kwa sababu ina kitenzi na maana kamili.

*20.*

- Thumni: Alinunua kiatu kwa thumni kubwa.
- Madhumuni: Madhumuni ya mkutano ni maendeleo ya shule.

*21.*

Nomino hizo huitwa nomino za dhana.



*22.*

Mwenda na omo marejeo ni mgeni.

*23.*

Mkate uli okwa vyema na kiwanda cha kutengeneza mikate.

*24.*

Nomino iliyo katika kundi tofauti ni:
Mimea

*25.*

Kama angeingia darasani mapema, angeandika insha.

*26.*

Mbinu ya lugha iliyotumika ni:
Sitiari

*27.*

Methali:
Kofi hazilii pweke.

FASIHI

28.

a)

Wimbo huu ni wa aina ya:
Wimbo wa kidini / Kikristo

b)

Sifa tatu za wimbo huu:

1. Unamsifu Mungu/Yesu
2. Una ujumbe wa imani na wokovu
3. Unatumia lugha ya kishairi

c)

Mazingira ambapo huimbwa:

1. Kanisani
2. Katika mazishi au ibada za kidini

d)

Mafunzo kuhusu Yesu:

- Yesu ni mwokozi
- Yesu huwapa watu amani
- Yesu huwasaidia wenye shida

e)

Mhusika mmoja:
Yesu

DONDOO

29.
a)

Mandhari inayojitokeza:
Mandhari ya huzuni na mateso

b)

Sifa tatu za mwandishi/mhusika:

1. Mwenye huzuni
2. Mwenye mawazo mengi
3. Mwenye matumaini kupitia kitabu chake

c)

Mafunzo matatu:

1. Kifo huleta maumivu makubwa
2. Maisha yana changamoto nyingi
3. Vitabu vinaweza kuwapa watu matumaini

d)

Mbinu tatu za lugha:

1. Taswira

2. Methali
3. Kurudia maneno



INSHA

Anwani ya Mwandikaji
S.L.P 234
Nakuru

29 Mei 2026

Rafiki yangu mpendwa Amina,

Shikamoo! Natumaini uko salama pamoja na familia yako. Mimi ni mzima wa afya na ninaendelea vyema na masomo yangu.

Ninakuandikia barua hii kukualika katika sherehe ya siku yangu ya kuzaliwa ambayo itafanyika Jumamosi ijayo tarehe 6 Juni 2026 nyumbani kwetu kuanzia saa nne asubuhi. Kutakuwa na chakula kitamu, muziki, michezo mbalimbali na burudani nyingi.

Nitafurahi sana ukihudhuria sherehe hiyo ili tusherekee pamoja kama marafiki wa karibu. Tafadhali fika mapema ili tushirikiane katika maandalizi ya shughuli mbalimbali.

Natumaini utaweza kuhudhuria. Wasalimie wazazi wako pamoja na ndugu zako wote.

Rafiki yako,
Cylus